

Swahili A: literature – Higher level – Paper 2
Swahili A : littérature – Niveau supérieur – Épreuve 2
Swahili A: literatura – Nivel superior – Prueba 2

Thursday 5 May 2016 (afternoon)
 Jeudi 5 mai 2016 (après-midi)
 Jueves 5 de mayo de 2016 (tarde)

2 hours / 2 heures / 2 horas

Instructions to candidates

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the part 3 works you have studied and compare and contrast these works in response to the question. Answers which are not based on a discussion of at least two part 3 works will not score high marks.
- You are not permitted to bring copies of the works you have studied into the examination room.
- The maximum mark for this examination paper is **[25 marks]**.

Instructions destinées aux candidats

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. En basant votre réponse sur au moins deux des œuvres de la troisième partie que vous avez étudiées, vous devez comparer et opposer ces œuvres dans le cadre du sujet. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la troisième partie n'obtiendront pas une note élevée.
- Vous n'êtes pas autorisé(e) à apporter des exemplaires des œuvres que vous avez étudiées dans la salle d'examen.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est de **[25 points]**.

Instrucciones para los alumnos

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Conteste una sola pregunta de redacción. Base su respuesta en al menos dos de las obras estudiadas de la parte 3, comparándolas y contrastándolas en relación con la pregunta. Las respuestas que no se basen en al menos dos obras de la parte 3 no recibirán una puntuación alta.
- No está permitido traer copias de las obras estudiadas a la sala de examen.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es **[25 puntos]**.

Jibu swali **moja** tu la insha. Jibu lako liegemee kwenye **angalau kazi mbili** za kazi za sehemu ya 3 ulizojifunza na ulinganishe kazi hizi kuabatana na swali. Majibu ambayo hayatahusisha mjadala wa kazi za sehemu ya 3 **hayatatunzwa** alama za juu.

Tamthilia

1. Mwanzo wa kila onyesho la tamthilia hutangulizwa na maelezo ya jukwaa ambayo hueleza mandhari ya onyesho. Huku ukilinganisha maelezo ya jukwaa ya angalau tamthilia zozote mbili ulizosoma, jadili umuhimu na mchango wake katika tamthilia hizo.
2. Jadili umuhimu wa maandishi kutumia majina ya kimajazi kwa wahusika kutoka angalau tamthilia zozote mbili ulizosoma na jinsi mbinu hii inafanikisha kueleza tabia za wahusika hao ili kufanikisha maudhui ya kazi hizo.
3. Huku ukirejelea angalau tamthilia mbili, linganisha jinsi maandishi walivyotumia mbinu ya uzungumzinafsiya kwa wahusika na umuhimu wake kufikisha ujumbe na kama wamefaulu au la na kwa njia gani.

Riwaya

4. Huku ukirejelea angalau riwaya mbili ulizosoma, eleza umuhimu wa matumizi ya mazungumzo/dayolojia katika usimulizi na athari zake katika kazi ya fasihi.
5. Linganisha angalau riwaya mbili ulizosoma jinsi maandishi walivyotumia kwa ufanisi vipengele vya utamaduni kama sehemu ya muktadha katika riwaya zao.
6. Huku ukirejelea angalau riwaya mbili ulizosoma, jadili matumizi ya ushirikina na jinsi unavyodokeza matukio yatakayojitokeza.

Ushairi

7. Ukirejelea angalau mashairi mawili uliyosoma, jadili jinsi washairi huvunja sheria za lugha na sarufi yake na kwa sababu gani.
8. Linganisha na ueleze matumizi ya lugha ya ishara ilivyotumika kutoka angalau mashairi mawili uliyosoma na ueleze ni vipi imechangia au kulemaza uelewekaji wa maudhui ya mashairi hayo.
9. Utata ni nini katika ushairi, na unajitokezaje katika angalau mashairi mawili tofauti uliyosoma? Linganisha na ulinganue maana zinazojitokeza katika mashairi hayo.

Riwaya ya mapenzi

- 10.** Kutoka angalau riwaya mbili za mapenzi za waandishi wawili au zaidi ulizosoma, ni jinsi gani mapenzi yanaathiriwa au kuchangiwa na utamaduni na itikadi za jamii husika?
 - 11.** Jadili tabia na athari za wahusika wengine kutoka angalau riwaya mbili za mapenzi ulizosoma na jinsi walivyochangia kufanikisha au kuporoposha mapenzi ya wahusika wengine.
 - 12.** Kuna mapenzi thabiti na mapenzi yasiyo na msingi imara. Ukirejelea angalau riwaya mbili ulizosoma, jadili sababu na matokeo ya aina hizi mbili za mapenzi na jinsi yanavyosaidia kukuza dhamira ya riwaya hizo.
-